BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 01 Machi, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

124. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Sheha ni kiungo muhimu sana katika kutoa huduma tofauti za Serikali kwa wananchi wa shehia zetu, lakini wanakabiliwa na changamoto tofauti ikiwemo ukosefu wa makatibu, vitendea kazi na ofisi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzitatua changamoto hizo.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

166. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kupitia Mradi wa 'Zanzibar Urban Services Project' (ZUSP), kuliwekwa taa za barabarani katika baadhi ya maeneo mengi kwa upande wa Unguja na Pemba. Lakini sasa hivi ukipita barabarani utaona taa nyingi haziwaki.

(a) Je, katika mikataba na wakandarasi hao, hakukuwepo na kipengele cha kufanyiwa ukarabati wa taa hizo.

(b) Kwa kuwa taa nyingi kati ya hizo hutumia umeme wa jua, je kuna mbadala wowote wa matumizi ya umeme wa ZECO kuendeshea taa hizo.

(c) Kama upo, je ni taasisi gani inahusika kulipia gharama za umeme, na bajeti yake inatoka katika fungu gani.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

137. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Suala la ubunifu katika mambo mbali mbali yenye maslahi na jamii lina nafasi gani katika kupiga hatua za maendeleo ya kiuchumi katika taifa letu.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani kwa sasa katika kuona kwamba suala la ubunifu kama zilivyo nchi zilizoendelea linalipa kipaumbele.

(b) Je, tuna wabunifu wangapi ambao wamebuni vitu vyenye maslahi na taifa letu lakini miradi yao imekwama kutokana na uhaba wa fedha.

(c) Je, Wizara haioni kuwa elimu ya ubunifu inahitajika kuanzia ngazi za chini za elimu, ili kuwandaa vijana wetu kuwa wavumbuzi wazuri.

Wizara ya Afya:

74. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wizara imekuwa ikipokea madaktari wa kujitolea wa magonjwa mbali mbali kutoka nje ya nchi ambao hutoa huduma zao kwa muda mfupi kwa kuweka kambi za uchunguzi. Suala hili hupelekea ukusanyaji wa wananchi ambao wana magonjwa mbali mbali ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

(a) Je, hatuoni kama tunahatarisha maisha ya wananchi wetu kwa kuwakusanya sehemu moja bila ya utaratibu maalum.

(b) Je, kuna ugumu gani unaopatikana kwa hospitali yetu ya Rufaa kuandaa kituo maalum cha kudumu kwa ajili ya uchunguzi utakaofanywa na madaktari wa kujitolea na kuweka utaratibu maalum wa uchunguzi huo, ili kukimbiza maambukizi yasiyo ya lazima kwa wananchi wetu.

(c) Ni nini hasa kinachopelekea kukosa kuwa na wahudumu wa afya ambao watahusika moja kwa moja na zoezi hilo kila inapotokea haja ya kufanya hivyo, ili kupunguza kuwachukua madaktari wa kusaidia kutoka vituo vyao vya kazi.

125. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujali wananchi wake kupitia Sekta ya Afya kwa ujenzi na uwekaji wa vitendea kazi vya kisasa katika wilaya tofauti za Zanzibar, lakini bado kuna uhaba mkubwa wa wataalamu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwezesha upatikanaji wa wataalamu katika hospitali hizo.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

156. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Pamoja na juhudi za Serikali katika kudhibiti mfumuko wa bei nchini, imeshuhudiwa kuwepo kwa bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula zilizoathirika na mfumuko huo, kiasi ya wananchi wetu kuendelea kupata shida ya maisha.

(a) Je, ni bidhaa gani za vyakula na zisizokuwa za vyakula ambazo zimeathiriwa na mfumuko mkubwa wa bei.

(b) Je, Wizara yako inachukua hatua gani za dharura pindi inapotokezea mfumuko wa bei ili kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha.

(c) Takwimu zikoje kwa sasa kuhusiana na changamoto hii ya mfumuko wa bei.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

77. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kuna dhamira iliyowazi ya kuboresha ustawi wa watu wenye ulemavu ili waweze kufurahia na kujumuika katika shughuli za kila siku bila ya kuwa na wasi wasi wala kuhisi kuwa wanabaguliwa. Pamoja na kwamba hali ya kuonekana kuwa ni mizigo katika taifa imeanza kupungua, bado kuna changamoto nyingi nyenginezo kielimu, kijamii na kiuchumi ambazo zinahitajika kutiliwa mkazo na kuangaliwa kwa jicho la karibu sana.

(a) Je, Zanzibar ina watoto wangapi wenye ulemavu ambao wanasoma katika Elimu Mjumuisho, Elimu Maalumu na ambao hawasomi na wamefikia umri wa kwenda skuli.

(b) Je, ni upi uwiano kati ya walimu na wanafunzi wa Elimu Mjumuisho (inclusive education).

(c) Je, ni ipi tathmini ya Serikali katika Elimu Mjumuisho Zanzibar.

134. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kuenea na kushamiri kwa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi kwa namna yoyote ile kunatokana na kukosa uzalendo na kutoipenda nchi yako.

(a) Je, Wizara ya Elimu inalizingatia vipi suala zima la mafunzo ya uzalendo kupitia maboresho mapya ya mitaala, ili iweze kuwaandaa mapema watoto wetu kuwa raia wema watakaokuja kutimiza majukumu yao.

(b) Je, njia zinazotumika hivi sasa kwa mfano kuimba wimbo wa taifa na wimbo wa mashujaa zinatosheleza kuwandaa vijana wetu kuja kuwa raia wema katika taifa lao.

(c) Ni athari gani kama taifa inapatikana kutokana na kukosekana uzalendo wa kweli.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

94. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu sasa, wananchi wa shehia ya Ngwachani, Kenya na Maweni hawapati maji ya ZAWA.

(a) Je, ni nini hasa tatizo la wananchi wa shehia hizo kukosa maji.

(b) Je, ni lini wananchi hao watapata maji.

143. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kila wakati wananchi wa Zanzibar wanatoa taarifa za ubovu au kupasuka kwa mabomba ya maji kwa watendaji husika wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), ili hatua za haraka zichukuliwe kunusuru upotevu wa maji. Hata hivyo, kumekuwa na uchelewaji kwa ZAWA kuchukuwa hatua za haraka za kurekebisha mabomba yaliyopasuka lakini wanakuwa na haraka kudai malipo ya kila mwezi.

(a) Ni sababu gani zinawafanya ZAWA wachelewe kurekebisha mabomba ya maji yanayopasuka kwa wakati na kusababisha upotevu wa maji.

(b) Kwanini ZAWA wasianzishe mfumo rahisi wa kutambua athari za miundombinu popote pale ilipo na kufika kwa wakati ili kurekebisha kasoro iliyojitokeza.

(c) Ni kiwango gani cha maji kinapotea kila mwaka kutokana na kupasuka kwa mabomba ya maji ya ZAWA.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

87. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wakulima wetu nchini wanaendelea kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa (mabadiliko ya tabianchi). Hali hii hupelekea kipindi cha jua kali, wakulima wanaotegemea kilimo cha mvua, kwa vyovyote

wanalazimika kuachana na kilimo kwa muda, kutokana na kukosekana kwa mvua hizo na jua kuwa kali sana.

Je, Serikali ina mpango gani kwa wakulima ambao kwa sasa wana umaskini na wanashindwa kulima ingawa ardhi wanayo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

102. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kukabiliana na majanga mbali mbali yanayotokea baharini yakiwemo yale ya uharamia wa kimataifa, viko vituo mbali mbali vilivyoanzishwa kupambana na hali hiyo, ambapo nchini mwetu Tanzania tunacho kituo kinachojuilikana kwa jina la 'Maritime Rescue Coordination Center' (MRCC) kilichopo Dar es Salaam.

(a) Je, Zanzibar inapata mashirikiano gani kupitia kituo hiki cha MRCC kilichopo Dar es Salaam.

(b) Kwa upande wetu hapa Zanzibar, je, tunacho kituo kinachotoa huduma zinazofanana na kituo hicho kwa mujibu wa utendaji wake wa kazi

(c) Kama kipo, je, kiko wapi na vipi kinatekeleza kazi zake.

103. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Moja kati ya ahadi zilizotolewa na Serikali yetu ya Awamu ya Nane, ni ile ya ujenzi wa bandari mjumuishi na ya kisasa huko Mangapwani. Kwa kuwa huu ni mwaka wa tatu umeingia, bado hakujawa na hatua yoyote ile ya ujenzi ukiacha tu ile ya upembuzi yakinifu.

(a) Je, ni lini hasa ahadi hii itatekelezwa.

(b) Je, Serikali haioni kuwa umepita muda mrefu tokea ahadi hii ilipotolewa kwa Wazanzibar, na bado haijatekelezwa hadi leo.

(c) Kwa kiasi gani wananchi wetu wameondokewa na matumaini ya kutekelezwa kwa ahadi.

IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taarifa ya Mapitio na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2023/2024.

Zanzibar,
01 Machi, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.